OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
(W),
S.L.P. 2,
KATESH-HANANG,
MANYARA.

31/10/2017
SIMU NA :027-2530022
25 30042
NUKUSHI NA : 027/2530022
: 027/2530042

TANGAZO LA ZABUNI

NAMBA YA ZABUNI. LGA/059/HQ/2017/2018/NC/10

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang inawatangazia Wananchi wote, watu binafsi na Makampuni kuomba Zabuni ya kukodisha shamba la Bassotu Plantation lenye ukubwa wa ekari elfu tisa (9,000/=) ambalo liko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. Manunuzi haya yanashirikisha jamii (community participation) kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 168 ya ununuzi wa Umma ya mwaka 2013.

Shamba liko kwenye eneo zuri lenye udongo wenye rutuba, Aidha shamba hilo linakodishwa kwa bei nzuri kwa ekari ambayo kila mwananchi ataweza kumudu kukodisha . Shamba hilo litakodishwa kwa vipimo vifuatavyo:

1. Kundi la Wakulima kuanzia ekari kumi (10) hadi mia moja (100).
2. Kundi la Wakulima kuanzia ekari mia moja na moja (101) hadi mia tatu (300).

MASHARTI YA ZABUNI

1. Mwombaji wa Zabuni wa kundi Na. 1 anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 20,000/= ambayo haitarudishwa hata kama mwombaji wa Zabuni hatateuliwa na mwombaji wa kundi Na.2 atalipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 50,000/= ambayo haitarudishwa na atapewa nyaraka za Zabuni “Tender Document” na Katibu wa Bodi ya Zabuni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri. Ada za maombi zilipwe kwa mtunza fedha wa Halmashauri “Cashier” siku za kazi Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi 8:00 adhuhuri.

2. Mwombaji atakayeshinda Zabuni ataingia Mkataba wa msimu moja tu kuanzia tarehe 01/12/2017 hadi tarehe 30/09/2018 na haruhusiwi kupanda mazao ambayo ukomavu/uvunaji wake utavuka msimu mwingine.
3. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atatakiwa kulitumia shamba hilo kwa shughuli za kilimo tu na siyo shughuli zingine kama vile ufugaji au uchungaji wa mifugo na ikiwa atafanya shughuli ambazo sio za kilimo Halmashauri itamnyang’anya shamba hilo bila kurejeshwa au kurudishiwa fedha za ukodishaji.

4. Ikiwa Mzabuni hatavuna mazao kutokana na hali ya hewa yaani ukame, mafuriko au wadudu waharibifu na mambo mengine ambayo yanafanana na haya, Halmashauri haitahusika na hasara hiyo.

5. Mzabuni anatakiwa kupanda mazao ambayo hayaleti uharibifu wa mazingira kulingana na Sheria inayotawala Mazingira.

6. Mzabuni ataje aina ya mazao anayohitaji kupanda katika eneo/shamba analoomba.

7. Mzabuni anatakiwa kutoharibu makinga maji “Contours” ambayo yapo katika shamba kwa kuyalima au kuyaondoa.

8. Halmashauri haitahusika na hasara itakayojitokeza katika kulima shamba atakalokodishiwa Mzabuni mfano:- ulinzi wa shamba, uharibifu unaotokana na mifugo na mengine yanafanana na hayo maana yake ni kwamba majukumu yote yanahusu shamba atakalokodishiwa ni juu ya Mzabuni kuanzia tarehe 01/12/2017 hadi tarehe 30/09/2018.

9. Mzabuni atatakiwa kulipa fedha zote za ukodishaji wa shamba ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupewa barua ya kukubaliwa na atapimiwa na kuoneshwa eneo lake ndani ya siku saba (7) baada ya kulipia.

10. Kama kutatokea kutoeleweka au kutoelewana katika utekelezaji wa sharti lolote la Mkataba utakaofungwa kati ya Halmashauri na mshindi wa Zabuni (Mkulima) pande zote mbili zitakaa na kutatua tatizo kwa njia ya majadiliano. Ikiwa majadiliano yatashindwa kuleta muafaka suala hilo litapelekwa kwa msuluhishi ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tawi la Katesh na ikiwa usuluhishi utashindikana shauri la suala hilo litapelekwa Mahakamani.

11. Mwombaji wa Zabuni anaweza kupewa idadi ya ekari alizoomba au kupewa pungufu kutegemeana na idadi ya waombaji katika kundi aliloomba.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:
KATIBU WA BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG,
S.L.P 2,
KATESH – HANANG.

1. ZABUNI YA UKODISHAJI SHAMBA LA BASSOTU PLANTATION – KUNDI NA. 1. **(Chagua kipengele hiki kama wewe ni mkulima wa kundi kuanzia ekari 10 – 100).**
2. ZABUNI YA UKODISHAJI SHAMBA LA BASSOTU PLANTATION – KIPIMO CHA WAKULIMA WAKUBWA. (**Chagua kipengele hiki kama wewe ni mkulima wa kundi kuanzia ekari 101 – 300).**
    - Wakulima wenye kuhitaji ekari moja (1) watakuwa katika kundi la ekari kumi ambapo watagawana kadri mwombaji anavyohitaji.
    - Namba ya kundi iandikwe juu ya bahasha.
    - Mwisho wa kuleta maombi na kupokea maombi ya Zabuni ni siku ya Jumanne tarehe 14/11/2017 saa 5:00 asubuhi kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang.
    - Maombi ya zabuni ambayo hayataletwa na kupokelewa na kusomwa siku ya ufunguzi hayatakubalika.
    - Maombi yote yapitishwe kwa Mtendaji wa Kijiji/ Mtendaji wa Kata.

BRYCESON P. KIBASSA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'

NAKALA:

1. Ofisi ya Katibu Tawala - Wilaya ya Hanang.
2. Watendaji wa Kata - Wajulisheni wakulima katika Kata zenu.
3. Watendaji wa Vijiji - Wajulisheni wakulima katika Vijiji vyenu.

BPK/ett.